

Muhtasari

- Vipindi vya hali ya ukavu vinavyotarajiwa vitasaidia katika shughuli za uvunaji na uhifadhi wa mazao. Hata hivyo hali hiyo inaweza kusababisha upungufu wa maji na malisho kwa mifugo.
- Wakulima wanashauriwa kuhifadhi ziada ya mavuno yaliyopita ili kuepuka upungufu wa chakula.
- Wakulima wanashauriwa kuanza maandalizi ya shamba kwa ajili ya msimu ujao wa vuli, hususan maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua.

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 21-31, 2018

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita (dekadi), migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo sehemu ya kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) ilikuwa imedhoofika kiasi. Ukanda wa mvua wa ITCZ uliendelea kubaki kaskazini ingawa kwa sehemu ilikuwa ikisogelea maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria kwa sababu ya kudhoofika kwa migandamizo ya hewa iliyopo kusini. Joto la bahari katika maeneo ya kusini magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa la wastani hadi chini ya wastani. Upepo ulivuma kutoka kusini mashariki hadi kusini katika maeneo mengi ya nchi. Eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kuliendelea kuwepo na joto la bahari la wastani hadi chini ya wastani hali iliyosababisha pepo hafifu kutoka magharibi na hivyo kudhoofisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 21-31, 2018

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita, sehemu kubwa ya nchi ilikuwa kavu isipokuwa vipindi vifupi vya mvua za nje ya msimu zilinyesha katika baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua hususan maeneo ya Pwani ya kaskazini na Kanda ya Ziwa Victoria ambapo yalipata mvua chini ya milimita 50.

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 21-31, 2018

Katika kipindi cha dekadini iliyopita shughuli za uvunaji wa mahindi zimemalizika maeneo mengi ya nchi isipokuwa maeneo yanayojishughulisha na kilimo cha pamba na mpunga, ambapo wakulima wanamalizia kuvuna.

Hali ya maji na malisho kwa ajili ya wanyama ilikuwa ya kuridhisha isipokuwa mikoa ya Dodoma na Tabora ambapo maji yameanza kupungua.

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 21-31, 2018

Kina cha maji katika mabwawa, mabonde na mtiririko wa maji katika mito ilikuwa ya wastani, isipokuwa bonde la Ziwa Victoria na Pangani ambapo hali ya maji inaonesha kuwa nzuri zaidi.

**MIFUMO YA HALI YA HEWA
INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA
SEPTEMBER 1-10, 2018**

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Ukanda wa mvua (ITCZ) unatarajiwa kuendelea kubaki kaskazini zaidi lakini sehemu yake inatarajiwa kuendelea kukaribia maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria. Pia pepo kutoka kusini mashariki zinatarijiwa kuendelea kuvuma katika maeneo ya ukanda wa pwani. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi hali itakayopunguza uwezekano wa kutokea kwa vimbunga baharini. Eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kunatarajiwa kuwa na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii itapelekea kupungua kwa upepo uvumao kutoka magharibi hivyo kupungua nguvu ya mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

**HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA
KIPINDI CHA SEPTEMBER 1-10, 2018.**

Katika kipindi cha siku kumi zijazo Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) inatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam maeneo ya kaskazini mwa Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) inatarajiwa kuwa na mvua katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi) na nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) yanatarajiwa kuwa na mawingu kiasi na makavu kwa ujumla.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kuwa na mawingu kiasi na makavu kwa ujumla.

**MATARAJIO NA USHAURI WA KILIMO KATIKA
KIPINDI CHA SEPTEMBER 1-10 2018.**

Hali ya ukavu inayotarajiwa itasaidia katika shughuli za uvunaji na uhifadhi wa mazao. Hata hivyo hali hiyo itasababisha upungufu wa maji na malisho. Wafugaji wanashauriwa kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na matumizi endelevu ya maji na malisho. Vilevile, wakulima wanashauriwa kuhifadhi akiba vizuri ziada ya chakula na kukitumia kwa uangalifu kuepuka upungufu wa chakula, hususan katika maeneo yote ambayo shughuli za uvunaji zimekamiliika.

Kwa maeneo yanayotarajia misimu miwili ya mvua, wakulima wanashauriwa kuanza kuandaa mashamba kwa ajili ya msimu ujao wa vuli unaotarajiwa kuanza hivi karibuni. Wakulima, wavuvi na wafugaji wanashauriwa kuwasiliana na maofisa ugani kwa ajili ya kupata ushauri zaidi.

**HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA
KIPINDI CHA SEPTEMBER 1-10, 2018.**

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuwa vya wastani katika sehemu nyingi nchini. Hata hivyo, wananchi wanashauriwa kutumia maji kwa uangalifu kwa matumizi endelevu ya rasilimali hii.

Jarida limetayarishwa na:

Mamiaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3-Ubungo Plaza - Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 - 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 - 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti:

www.meteo.go.tz